**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA**

# TAARIFA YA MWENYEKITI WA HALMASHAURI MKUTANO WA KAWAIDA WA BARAZA LA MADIWANI TAREHE 29/04/2022 KATIKA KIPINDI CHA ROBO YA TATU MWAKA WA FEDHA 2021/2022.

- Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Siha,
- Mwakilishi Ofisi ya RAS-Mkoa wa Kilimanjaro,
- Mh. Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Siha,
- Mhe. Makamu Mwenyekiti Halmashhauri ya Siha
- Waheshimiwa Madiwani,
- Ndugu Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Siha (Katibu wa Baraza),
- Wah Viongozi wa Madhehebu ya Dini,
- Wageni Waalikwa,
- Ndugu Wataalamu,
- Waandishi wa Habari,
- Wananchi wa Wilaya ya Siha,
- Mabibi na Mabwana,

Nawasalimu wote kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,napenda kumshukuru Mungu tena kwa Baraka zake za kutufikisha tena kipindi hiki cha robo ya tatu ya mwaka wa Fedha 2021/2022 huku tukiwa wazima wa afya njema. Kabla sijaendelea na taarifa yangu naomba tusimame kwa Dakika moja ili kuwakumbuka watumishi wawili na wananchi wote wa Wilaya ya Siha waliotangulia mbele za haki katika kipindi cha mwezi Januari hadi Machi 2022 **MUNGU AWAWEKE MAHALI PEMA PEPONI AMINI.**

Baada ya sala hiyo fupi napenda kuchukua nafasi hii adhimu na ya kipekee mbele ya baraza tukufu la Wah Madiwani Halmashauri ya Wilaya ya Siha **leo tarehe 29/04/2022** kutoa shukrani za dhati kwa Serikali yetu tukufu ya awamu ya Sita inaongozwa na mhe.SAMIA SULUHU HASSAN Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi anavyofanya juhudi kubwa kuhakikisha kuwa Wananchi wa Tanzania wanapata maendeleo.

Vile vile napenda kukishukuru Chama changu cha Mapinduzi (CCM) kwa jinsi kinavyoendelea kusimamia Serikali iliyopo madarakani na kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma stahiki tena kwa haraka katika maeneo yote ya Wilaya ya Siha.

Aidha, napenda pia kuwashukuru **Wah. Madiwani wote** wa Halmashauri ya Siha kwa ushirikiano wenu wa dhati na jinsi mnavyoshiriki katika kuhamasisha shughuli za maendeleo katika Kata.

Napenda kuwashukuru Wananchi,Viongozi na Watumishi wote katika Halmashauri ya Wilaya ya Siha kwa jinsi mnavyoendelea kuunga mkono juhudi za Rais wetu mama Samia Suluhu Hassan za Kuhakikisha kuwa Tanzania inabadilika na kupata maendeleo ya kweli kwa kila mmoja wetu kushiriki katika ujenzi wa uchumi kwa kipato cha Familia na Taifa kwa ujumla.

**Wah. Madiwani , na Ndugu Wananchi,**

Kama mnavyojua katika kipindi cha robo ya tatu Serikali yetu ya awamu ya Sita chini ya Rais wetu mpendwa mhe. SAMIA SULUHU HASSAN imeendelea kumimina fedha nyingi za maendeleo katika Halmashauri yetu ambapo katika robo hii ya tatu tumepokea shilingi milioni 800 kwa ajili ya Hospital yetu ya Wilaya ya Siha pamoja na shilingi milioni 150 kwa ajili ya Zahanati za **Messe,Mwangaza na Embukoi Hii ikiwa kila Zahanati imepata milioni 50**. Sisi kama Madiwani tunamshukuru pia Mbunge wetu wa Jimbo la Siha ambaye pia ni Naibu Waziri wa Afya kwa jinsi

anavyoendelea kutuwakilisha vema katika Bunge na kuhakikisha kuwa Serikali inaendelea kuleta fedha nyingi za Miradi ya maendeleo.

Pamoja na Serikali kuleta fedha nyingi za maendeleo napenda kumpongeza Mkurugenzi Mtendaji na Wataalam wake kwa usimamizi mzuri wa fedha katika kutekeleza miradi bora na imara ya maendeleo ila naomba tuendelee hivyo hivyo na kamwe tusilewe sifa nyingi tunazopewa na Viongozi wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Siha kuonekana kuwa na miradi bora na imara ya maendeleo. **MAMA SAMIA HOYEEEEEEEEE**

**Wah. Madiwani , na Ndugu Wananchi,**

Katika taarifa yangu kwa kipindi cha Robo ya Tatu yapo mambo muhimu nimeona niyazungumzie kama sehemu ya kusisitiza katika kipindi hiki kabla ya kumaliza mwaka wa fedha 2021/2022. Miongoni mwa masuala machache yaliyopo katika taarifa yangu ni pamoja na suala la **Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani ya Halmashauri,Kilimo,Uwajibikaji na Maadili kwa jamii ,Utekelezaji wa Miradi ya maendeleo Utunzaji wa Mazingira.**

## A. UKUSANYAJI WA MAPATO

**Waheshimiwa Madiwani, Ndugu Wananchi**

Napenda kuendelea kuhimiza Wataalam wetu kuendelea kufanya kazi kwa bidii zaidi ya ukusanyaji wa Mapato ya Ndani ya Halmashauri kama msingi wa uendeshaji wa Halmashauri pamoja na uboreshaji wa utoaji wa huduma bora kwa Wanachi wetu ,Wah Madiwani wote mtakuwa mashahidi kuwa Halmashauri yetu imekuwa ikitoa fedha nyingi za kukamilisha miradi ya maendeleo kama sehemu ya kuunga mkono juhudi za Wananchi pale wanaposhindwa kukamilisha miradi mbalimbali waliyoanzisha mfano mzuri ni Ukamilishwaji wa Zahanati ya Messe,ujenzi wa vyoo Loiwang,Shule ya Msingi Neema na Maeneo mengine mengi katika Halmashauri yetu. Napenda kuwajulisha Wah. Madiwani na Wananchi wa Halmashauri ya Siha kuwa katika kipindi cha robo ya Tatu Halmashauri yetu imetumia zaidi ya shilingi milioni 145 ya makusanyo yake ya ndani katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ndani ya Wilaya ya Siha.

Ni ukweli usiopingika kuwa kama tusingekuwa na ukusanyaji mzuri wa mapato ya ndani ya Halmashauri mambo haya mazuri ya maendeleo

tusingeweza kuyafanikisha kwa kiwango cha juu kama tulivyofanya na hivyo natoa rai kwa Wah. Madiwani wote kuendelea kubuni vyanzo vipya vya mapato na kusimamia vema fedha zote zinazokusanywa kutumika vizuri kwa manufaa ya wananchi wa Wilaya ya Siha na Watanzania kwa ujumla wake. Nimepata taarifa ya ukusanyaji wa mapato hadi kipindi cha robo ya tatu kuwa ukusanyaji wa mapato ya ndani umefikia shilingi Bilioni 1.3 sawa na asilimia 90.1 ya lengo jambo ambalo ni zuri na lina afya njema kwa Halmashauri yetu, naomba tumpongeze kwa dhati Mkurugenzi Mtendaji, CMT pamoja na wataalam wa Halmashauri kwa ujumla kwa kazi nzuri waliyoifanya, naomba kuwapongeza sana tena Halmashauri yetu pamoja na changamoto nyingi tulizopitia za ukame katika maeneo mengi ya Wilaya yetu yaliyosababisha kukosa mavuno ya msimu wa vuli na hivyo kukosekana kwa mazao.

Naomba kutoa wito wa usimamizi na ufuatiliaji zaidi wa mapato katika stendi yetu ya KIA kwani mimi na baraza la Madiwani tunaliona eneo hili kama eneo la kimkakati na kama chanjo muhimu na cha kudumu katika mapato ya ndani ya Halmashauri

Naomba kutoa msimamo wa baraza kuwa,Sisi kama baraza la Madiwani katika Halmashauri ya Siha hatutakuwa na mzaha au kupepesa macho kwa mtumishi yeyote atakayebainika kuhujumu na kutumia fedha za Serikali kwa maslahi yake binafsi,Tumeona tuseme haya mapema ili baadaye wakati wa utekelezaji tusilaumiane.

Aidha, katika kipindi cha robo ya tatu Januari hadi Machi 2022 Halmashauri yetu imetoa mikopo kwa vikundi vya Wanawake,Vijana na Watu wenye ulemavu yenye thamani ya shilingi milioni 97 kwa mchanganuo ufuatao:- **Vikundi vya Wanawake shilingi milioni 63.68,Vikundi vya Vijana shilingi milioni 23.06 na Vikundi vya Watu wenye ulemavu shilingi milioni 10.97**

**Wah. Madiwani na Ndugu Wananchi**

Kwenye fedha za miradi ya maendeleo naomba kutoa shukrani za dhati kwa mhe. Godwin Mollel Mbunge wa jimbo la Siha na Naibu Waziri wa afya kwa jitihada zake kubwa za kutuwakilisha vema na kuhakikisha Halmashauri yetu inapata fedha za maendeleo. Sisi kama baraza la madiwani tunaahidi kuendelea kushirikiana naye bega kwa bega katika maendeleo ya Wilaya ya Siha. Napenda kutoa shukrani za dhati kwa

Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi inavyotupatia fedha nyingi za kutekeleza miradi ya maendeleo .

**Waheshimiwa Madiwani,Ndugu Wananchi**

B. **KILIMO.** Napenda kumshukuru Mungu kwa Neema ya Mvua za masika tuliyoipata hivi karibu katika maeneo mengi ya Wilaya yetu japo hadi sasa bado tunayo baadhi ya maeneo katika Wilaya yetu yanapata mvua chache sana na mengine hayajapata mvua kabisa. Kwa hali hii naomba kutoa wito kwa wananchi wetu kuendelea kusikiliza ushauri wa wataalam wa kilimo pamoja na kubadilika na kuanza kuotesha mazao yanayostahimili ukame kama vile alizeti,mtama na mihogo japo kwa baadhi ya wananchi wetu hawajazoea mazao hayo.

Vilevile, napenda kuwaomba wananchi wetu katika Halmashauri ya Wilaya ya Siha kutumia vizuri chakula kilichopo hadi hapo msimu utakapomalizika na wataalam wetu watakapoweze kufanya tathmini na kujua hali ya chakula katika maeneo yote ya Wilaya yetu. Naomba wale waliopata mvua katika maeneo yao basi watumie mvua hizo vizuri katika kuhakikisha kuwa wanapata mazao bora na kuboresha hali ya kipato katika Familia ,Wilaya na Taifa kwa ujumla.

**Waheshimiwa Madiwani na ndg Wananchi;**

## C. **UWAJIBIKAJI NA MAADILI**

Wah. Madiwani na Wananchi wa Wilaya ya Siha naomba kuwaomba na kuwataka Watumishi wa Serikali katika Halmashauri yetu kuendelea kuchapa kazi ya kutoa huduma bora kwa Wananchi wetu kwa kutumia taaluma zao walizoajiriwa nazo na kwa upande wetu sisi Madiwani wa Halmashauri ya Siha tutawapa ushirikiano wa kila hali ili kufanikisha malengo ya Serikali ya awamu ya Sita.

Kipekee napenda kuwapongeza na kuwashukuru Watumishi wa Halmashauri yetu kweli wanajitahidi kufanya kazi na kutoa huduma bora kwa wananchi na hata kama kuna malalamiko basi ni kwa baadhi ya maeneo machache tu.

Kuhusu matukio mbalimbali yakusikitisha ya mauaji ya watoto wadogo wawili yaliyotea hivi karibuni katika Kata ya Songu na Makiwaru naomba kutoa wito kwa viongozi wetu wa madhehebu ya dini ,viongozi wa Kisiasa pamoja na wazazi na walezi kuendelea kusisitiza watu kuishi kwa maadili mema katika jamii. Jambo hili ni jambo kubwa kwetu lakini najua vyombo husika vinavyosimamia usalama vinafanya kazi zao na sisi kama raia

ambao ni walinzi wa usalama namba moja tunatakiwa kutunza usalama wetu na kuwafichua wale wote wanaonekana kwenda kinyume na mila,desturi na tamaduni zetu.

## D. **UTUNZAJI WA MAZINGIRA**

**Wah. Madiwani,Wananchi na Waandishi wa Habari**

Napenda pia kuwaomba Wananchi katika Halmashauri ya Wilaya ya Siha kuwa, kutokana na mabadiliko ya Tabia Nchi tunayoiona sasa ambayo wataalam wengi duniani wanasema imetokana na shughuli za kibinadamu hususani uharibifu wa mazingira unaotokana na ukataji wa miti pamoja na ukuaji wa viwanda vikubwa katika mataifa yaliyoendelea. Naomba kutoa wito kwa wananchi wetu kuotesha miti walau 5 kila mwaka kwa kila kaya kwani kwa sasa tunazo taasisi nyingi zinatoa miti bure kwa Wananchi ziliwemo **TFS, FRORESTA na Kikundi cha MATONYOK kilichopo Kata ya Livishi** kijiji cha Samaki . Pia naomba Halmashauri yetu kutumia vema bustani yetu ya kitalu cha miti iliyopo Kata ya Nasai na kuhakikisha kuwa Halmashauri inatenga bajeti ya kutosha kila mwaka katika kuzalisha miche ya miti ya kutosha na kugawa bure kwa Taasisi zinazosimamiwa na

Halmashauri na kwa Wananchi wetu kama ilivyokuwa hapo miaka michache iliyopita.

Napenda kusema usemi uliosemwa na mhifadhi wa misitu tarehe 26.4.2022 katika sherehe za miaka 58 ya Muungano pale Hospital ya Wilaya ya Siha kuwa "**MITI INAWEZA KUWEPO BILA SISI BINADAMU,LAKINI HAKUNA UHAI KAMA HAKUNA MITI** ".

Naomba kama inawezekana basi tuanzishe mashindano ya kila Kata ya upandaji miti na utunzaji wa mazingira kwa wananchi wetu kwa kila mwaka na matokeo ya kila mwaka yatolewe kwa kutajwa kata ya kwanza hadi ya mwisho na zawadi mbalimbali kutolewa kwa mshindi.

Wazo hili naomba kuliacha kwa Mkurugenzi na Timu yake walifanyie kazi na kuleta mrejesho katika vikao na mikutano mbalimbali kwa utekelezaji.

Mwisho kabla ya kumaliza taarifa yangu napenda nitoe shukrani za dhati kwa wafuatao:-

i)Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya **mhe. Samia Suluhu Hassan Rais Mzalendo Mbunifu na Mchapakazi no moja**

ii)Naibu Waziri wa afya na Mbunge wetu wa jimbo la Siha **mhe. Dkt. Godwin Mollel** kwa jitihada zake kubwa za kufuatilia na kuhakikisha Serikali inatupatia fedha za miradi ya maendeleo katika Wilaya yetu.

iii)Mhe. Thomas Apson Mkuu wetu wa Wilaya ya Siha kwa namna anavyosimamia shughuli za Serikali hususani katika ulinzi na amani pamoja na kusikiliza na kutatua kero mbalimbali za wananchi katika Wilaya yetu

iv)Viongozi wa Chama cha Mapinduzi ngazi ya Wilaya ,Kata na ngazi za chini waliongozwa na Mhe. Wilfred Mosi(Baba Lao) kwa namna wanavyosimamia utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya **CCM 2020-2025**

**wah Madiwani ,ndugu Wananchi**

Mwisho kabisa ,Napenda kuwashukuru kwa namna ya pekee wananchi wangu wa Kata ya Karansi kwa jinsi wanavyoendelea kuniamini na kuniombea afya njema katika nafasi yangu ya Udiwani,Napenda kuwaambia kuwa sintawaangusha.

Vilevile nawashukuru tena Wah. Madiwani wenzangu pamoja na Watumishi wa Serikali katika Halmashauri ya Siha kwa jinsi mnavyochapa kazi kwa kujituma,naomba ushirikiano uliopo uendelee daima siku zote kwa

maendeleo ya Wananchi wa Wilaya ya Siha. Nawashukuru pia Wananchi na Wakazi wa Siha kwa usikivu wenu mkubwa mlionesha tangu mwanzo wa taarifa yangu hadi sasa ninapohitinisha taarifa yangu, naomba usikivu na utulivu huu uendelee hadi mwisho wa Mkutano wetu.

**Mungu ibariki Tanzania,Mungu ibariki   Wilaya yetu ya Siha**

Asanteni sana kwa kunisikiliza

**Imetolewa na:**

**Mhe. Duncan B. Urassa**

Mwenyekiti wa Halmashauri (W)

**SIHA**